



MRADI WA 'SIMPLIFIED SEWERAGE' WAIBUKA KINARA **uk 2**

■ Kwa miradi inayotekelezwa kupitia mfuko wa EU-AITF



Mfumo wa Majitaka

Mhandisi Anthony Sanga

DC NYAMAGANA AIPONGEZA MWAUWASA

uk 10

Mwauwasa wapigwa msasa na Jumuiya ya kimataifa ya maji

uk 3



MRADI WA 'SIMPLIFIED SEWERAGE' WAIBUKA KINARA

Mradi wa Majitaka unaotekelezwa kwenye maeneo ya miinuko Jijini Mwanza unaofahamika kama "Simplified Sewerage" umekuwa miongoni mwa miradi miwili bora zaidi kuwahi kutekelezwa Barani Afrika chini ya ufadhili wa African

Infrastructure Trust Fund (EU-AITF).

Hayo yameelezwa mwishoni mwa Mwezi Novemba, 2018 wakati wa Mkutano wa kujadili miradi inayofadhiliwa na Benki ya Uwekezaji ya Ulaya (EIB) kupitia mfuko huo wa EU-AITF.

Katika mkutano huo ilielezwa kwamba tangu mfuko huo uanzishwe mnamo mwaka 2007 ni miradi miwili pekee ambayo imefuzu na kuwa miradi bora zaidi kuwahi kutekelezwa ambayo ni Mradi wa Majitaka wa Simplified Sewerage wa Jijini Mwanza, nchini Tanzania na mwingine ni mradi wa Nishati ya Umeme wa Benin & Togo.

Akizungumzia mradi wa Majitaka wa Jijini Mwanza, Mshauri wa masuala ya Kiufundi wa Benki ya Uwekezaji ya Ulaya, Raoul Pedrazzani alielezea hali ilivyokuwa hapo awali kabla ya kujengwa kwa mradi mpya wa majitaka kwenye maeneo ya milimani jijini humo.

Pedrazzani alisema kuwa kijiografia maeneo mengi ya Jiji la Mwanza ni milima/miinuko na kabla ya mradi huo wa majitaka wakaazi wa maeneo ya milimani hawakuwa na mfumo mzuri wa uondoaji wa majitaka.

Alisema suluhisho ilikuwa ni kubuni mradi ambao utarahisisha uotoaji wa majitaka kutoka kwenye makazi hayo kwenda yanakostahili.

Kwa upande wake Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Jijini Mwanza (MWAUWASA), Mhandisi Anthony Sanga alithibitisha kupokea ujumbe wa pongezi juu ya ushindi huo.

Mhandisi Sanga aliipongeza Bodi ya Wakurugenzi ya MWAUWASA kwa usimamizi mahiri wa shughuli zinazotekelezwa na Mamlaka na pia aliwapongeza watumishi wote wa MWAUWASA kwa utekelezaji na usimamizi mzuri wa miradi husika. "Mungu ni Mwema, tunamuomba Aendelee kutusaidia. Hakika kwa pamoja tunaweza," alisema Mhandisi Sanga.

Aliongeza kuwa lengo la Serikali ni kuhakikisha huduma ya majitaka inapanuka zaidi ili wananchi walio wengi waweze kufikiwa.

Maeneo ya miinuko ambayo tayari yamefikiwa na mfumo huo wa 'Simplified Sewerage' ni Kilimahewa, Mabatini na Igogo na huku lengo likiwa ni kupanua wigo na kufikia maeneo mengi zaidi.



Moja ya eneo lililofikiwa na mfumo wa majitaka ujulikanao kama 'Simplified Sewerage'. Pichani ni Mtaa wa Unguja, Kata ya Mabatini Jijini Mwanza ambalo limenufaika kupitia ufadhili wa African Infrastructure Trust Fund (EU-AITF).



Mwauwasa wapigwa msasa na Jumuiya ya kimataifa ya maji

Watumishi wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Jijini Mwanza (MWAUWASA) wame-takiwa kuzingatia Mpango wa Usalama wa Maji kila wanapotekeleza shughuli zao ili kuhakikisha wananchi wanapata maji safi na salama kwa ubora unaotakiwa.

Wito huo ulitolewa Novemba 12, 2018 na Mkurugenzi Mtendaji wa MWAUWASA, Mhandisi Anthony Sanga wakati wa ufunguzi wa mafunzo ya uandaaji wa Mpango wa Usalama wa Maji yanayotolewa kwa wafanyakazi wa MWAUWASA na Jumuiya ya Kimataifa ya Maji (IWA).

Mhandisi Sanga alisisitiza umakini kwenye usimamizi wa mnyororo mzima wa utoaji huduma ya maji kuanzia kwenye chanzo, uzalishaji hadi yanapomfikia mtumiaji ambapo alisema ni wajibu wa kila mtumishi kuhakikisha maji yanayozalishwa yana ubora unaokubalika Kitaifa na Kimataifa.

Aliongeza kuwa suala la usalama wa maji ni nyeti na linapaswa

kupewa kipaumbele cha kipekee na kila mtumishi ili kutimiza wajibu wa kuwapatia wananchi huduma wanayostahili kupata.

“Watumishi mliopata nafasi ya kuhudhuria mafunzo haya, mkitoka hapa hakikisheni mnawaelimisha na wale ambao hawakufanikiwa kushiriki,” alisema Mhandisi Sanga.

Aliwataka waliohudhuria mafunzo hayo kuuliza maswali na kufuatilia kwa umakini ili mara baada ya mafunzo hayo waboreshe Mpango wa Usalama wa Maji uliopo.

Mafunzo hayo ya siku Tano yalianza Tarehe 12 Novemba, 2018 na yalimalizika Tarehe 16 Novemba, 2018 lengo likiwa ni kuwawezesha wataalam wa MWAUWASA kuhakikisha ubora wa maji wanayosambaza kwa wananchi kuanzia mahala yanapozalishwa hadi yanapofika kwa mtumiaji.

Kwa mujibu wa Mkufunzi kutoka IWA, Kizito Masinde alisema MWAUWASA ndiyo Mamlaka pekee miongoni mwa Mamlaka za Maji Nchini ambayo imepewa kipaumbele cha mafunzo hayo.

Kizito aliongeza kwamba matarajio ya IWA ni kuona wataalam wa MWAUWASA wakitoa mafunzo ya namna hiyo kwa Mamlaka zingine kote nchini.



Washiriki wa mafunzo ya uandaaji wa Mpango wa Usalama wa Maji yanayotolewa na Jumuiya ya Kimataifa ya Maji (IWA) wakifuatilia mafunzo.

BODI YA UHARIRI

Mohamed Saif
Assistant
Manager Public
Relations
MWAUWASA

Ikupa Enock
Graphic Designer



LIMETOLEWA NA:

Mamlaka ya Majisafi
na Usafi wa Mazingira
Jijini Mwanza
(MWAUWASA).



0800110023



mwaumasatz



mwaumasat



Ziara ya Bodi na Menejimenti ya Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mjini Moshi (MUWSA) Jijini Mwanza.

Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Jijini Mwanza (MWAUWASA) imezindua kampeni yake inayokwenda kwa jina la 'Zungumza na MWAUWASA' ambayo imelenga kubaini kero mbalimbali za maji zinazowakabili wananchi wa maeneo mbalimbali Jijini Mwanza na viunga vyake sambamba na kutoa elimu ya maji kwa wananchi.

Kampeni hiyo ilizinduliwa rasmi na Meneja Biashara wa MWAUWASA, Meck Manyama kwa niaba ya Mkurugenzi Mtendaji wa Mwauwasa, Mhandisi Anthony Sanga hapo Novemba 6, 2018 kwenye Mitaa ya Dkt. Shein na Mkapa katika Kata ya Igoma.

Programu ilianza kwa kuzungumza na wananchi ambapo changamoto mbalimbali zilijadiliwa kwa lengo la kupata ufumbuzi wa pamoja.

"Tunaelewa zipo changamoto nyingi kwenye suala la maji, na ndiyo maana tumekuja na kampeni hii ili tumfikie kila mwananchi kwa lengo la kutafuta ufumbuzi wa pamoja," alisema Manyama.

Manyama alisema kampeni hiyo ni endelevu na kwamba imeanzia kwenye mitaa ya Dokta Shein na Mkapa kwenye Kata ya Igoma na itafanyika kwa mitaa yote kwa mtindo wa mikutano ambapo wananchi watapata fursa ya kueleza kero zinazowakabili kuhusiana na suala zima la maji.

Aliongeza kuwa kupitia kampeni hiyo, wananchi watapatiwa elimu ya masuala mbalimbali yanayohusiana na maji ikiwemo matumizi bora ya maji, ulipaji wa Ankara, uwasilishaji wa kero huku lengo likiwa ni kuwaongezea uelewa wa shughuli zinazotekelezwa na MWAUWASA.

Wataalam mbalimbali kutoka MWAUWASA walihudhuria mkutano huo kwa lengo la kujibu maswali ya wananchi sambamba na kupokea maoni.

IGOMA WAZUNGUMZA NA MWAUWASA





Matukio mbalimbali katika picha



Mkurugenzi Mtendaji wa MWAUWASA, Mhandisi Anthony Sanga (kulia) akizungumza wakati wa ufunguzi wa mafunzo ya uandaaji wa Mpango wa Usalama wa Maji yanayotolewa kwa wafanyakazi wa MWAUWASA na Jumuiya ya Kimataifa ya Maji (IWA).



Baadhi ya washiriki wa mafunzo ya uandaaji wa Mpango wa Usalama wa Maji yanayotolewa na Jumuiya ya Kimataifa ya Maji (IWA) wakimsikiliza Mkufunzi Kizito Masinde (hayupo pichani).



Baadhi ya washiriki wa mafunzo ya uandaaji wa Mpango wa Usalama wa Maji yanayotolewa na Jumuiya ya Kimataifa ya Maji (IWA) wakimsikiliza Mhandisi Anthony Sanga (hayupo pichani). Wa pili kulia ni Mkufunzi kutoka IWA, Kizito Masinde.



Washiriki wa mafunzo ya uandaaji wa Mpango wa Usalama wa Maji yanayotolewa na Jumuiya ya Kimataifa ya Maji (IWA) katika picha ya pamoja na Mkurugenzi wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Jijini Mwanza (MWAUWASA), Mhandisi Anthony Sanga (mbele katikati) mara baada ya ufunguzi wa mafunzo.



Mjumbe wa Bodi ya Wakurugenzi ya Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira (MWAUWASA), Denisa Pagula (kushoto) akizungumza na wafanyakazi wa Mamlaka (hawapo pichani). Pembeni yake ni Mjumbe wa Bodi, Edith Mudogo na Mkurugenzi Mtendaji wa MWAUWASA, Mhandisi Anthony Sanga.



Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, John Mongella (katikati waliokaa) katika picha ya pamoja baadhi ya wafanyakazi wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Jijini Mwanza wakati wa hafla ya kukabidhi zawadi kwa watumishi wa Kanda ya Makongoro iliyoshinda kiutendaji. Kushoto kwake ni Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya MWAUWASA, Christopher Gachuma na Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka hiyo, Mhandisi Anthony Sanga. Kulia kwake ni Wajumbe wa Bodi ya Mamlaka, Edith Mudogo na Denisa Pagula.



TUMETEKELEZA NANSIO NA TUNATEKELEZA LAMADI



Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. John Pombe Magufuli na Waziri wa Maji, Mhe. Profesa Makame Mbarawa na viongozi wengine wakisikiliza maelezo ya mradi wa maji wa Nansio Ukerewe yaliyokuwa yakitolewa na Mkurugenzi wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Jijini Mwanza (MWAUWASA), Mhandisi Anthony Sanga.



Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. John Pombe Joseph Magufuli akimsikiliza Waziri wa Maji, Profesa Makame Mbarawa mara baada ya kukagua pampu za kusukuma maji kwenye mradi wa maji wa Nansio Ukerewe wakati wa uzinduzi wa mradi huo Tarehe 04 Septemba 2018.



Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. John Pombe Magufuli akiweka Jiwe la Msingi la Mradi wa Maji wa Lamadi mkoani Simiyu Septemba 08, 2018 unaosimamiwa na Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Jijini Mwanza (MWAUWASA). Mradi utazalisha lita Milioni 3.3 za maji kwa siku mara baada ya kukamilika.

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli (kulia) akisalimiana na Wakandarasi wa mradi wa maji wa Lamadi mara baada ya kuwasili kwa ajili ya kuweka jiwe la msingi la mradi huo Septemba 08, 2018. Mradi unasimamiwa na Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Jijini Mwanza (MWAUWASA).





Waziri wa Maji, Mhe. Profesa Makame Mbarawa akikata utepe kuzindua rasmi matumizi ya mita za malipo kabla kwa huduma ya maji jijini Mwanza.

YALIFANYIKA 2018..

- WAZIRI WA MAJI, PROFESA MAKAME MBARAWA...
- AZINDUA RASMI MATUMIZI YA MITA ZA MALIPO KABLA
- AZINDUA JENGO LA MAJI HOUSE
- AKAGUA MRADI WA MAJITAKA



Waziri wa Maji, Mhe. Profesa Makame Mbarawa akiangalia mfumo wa Dira za malipo kabla ya huduma ya maji, mara baada ya kuzindua matumizi ya mita hizo, jijini Mwanza.



Waziri wa Maji, Mhe. Profesa Makame Mbarawa akikagua ubunifu uliotumika katika ujenzi wa mradi wa maji taka, Mabatini mtaa wa Unguja wilaya ya Nyamagana. Mradi huo umejengwa katika vilima na umesaidia kuondosha uchavuzi wa mazingira na magonjwa ikiwamo Kipindupindu.



Waziri wa Maji, Mhe. Profesa Makame Mbarawa akipewa maelezo kuhusu dash board yenye taarifa mbalimbali kuhusu huduma kwa wateja na uwajibikaji katika Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira jijini Mwanza (MWAUWASA)



Waziri wa Maji, Mhe. Profesa Makame Mbarawa akifungua rasmi jengo la Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira jijini Mwanza (MWAUWASA), Maji House.



Sehemu ya watumishi wa Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira jijini Mwanza (MWAUWASA) wakimsikiliza Waziri wa Maji, Mhe. Profesa Makame Mbarawa (hayupo pichani).



Waziri wa Maji, Mhe. Profesa Makame Mbarawa akipewa maelezo kuhusu dash board yenye taarifa mbalimbali kuhusu huduma kwa wateja na uwajibikaji katika Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira jijini Mwanza (MWAUWASA).

Waziri wa Maji Mhe. Profesa Makame Mbarawa (Mb) akiongea na baadhi ya wakazi wa Mabatini, mtaa wa Unguja, jijini Mwanza walionufaika na mradi wa Maji taka. Mradi huo umewaondolea wananchi adha ya uchafuzi wa mazingira na magonjwa, hususan kipindupindu.

Waziri wa Maji Mhe. Profesa Makame Mbarawa (Mb) katika picha ya pamoja na wakazi wa Mabatini, mtaa wa Unguja walionufaika na mradi wa Maji taka. Mhe. Mbarawa amehidi kila mkazi kuunganishwa katika mradi huo.






WANAFUNZI KITANGIRI WAIPONGEZA MWAUWASA



Moja ya choo kilichojengwa na MWAUWASA kwenye Shule ya Msingi ya Kitangiri. Choo hicho kimejengwa kwa ufadhili wa Benki ya Uwekezaji ya Ulaya (EIB), Shirika la Maendeleo la Ufaransa (AFD) na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

EDMUND EDWARD

**DARASA LA TANO,
SHULE YA MSINGI KITANGIRI**
Tunawashukuru MWAUWASA kwa kutujengea vyoo vya kisasa kwani vimetusaidia kuwa katika hali ya usafi muda wote. Hapo awali tulikuwa tunajisaidia vichakani kwakuwa hatukuwa na vyoo vya kutosha. Ninaishauri jamii ijenge vyoo bora na wajiunge na mfumo wa majitaka waache tabia ya kusubiri mvua inyeshe ndio wafungulie majitaka kwani hali hiyo inahatarisha afya zetu.



Wanafunzi wa Shule ya Msingi Kitangiri wakinawa mikono mara baada ya kutoka chooni. Vyoo hivyo vya kisasa vimeungwa na mfumo wa huduma ya majisafi ambao unawawezesha wanafunzi hao kujisafisha vizuri na hivyo kuepuka maradhi.

NURU ALLY

**DARASA LA TANO,
SHULE YA MSINGI KITANGIRI**
Maji ni muhimu sana katika maisha ya binaadamu, bila maji hakuna uhai. Hapo zamani hapa shuleni, wanafunzi walikuwa wakijisaidia pembeni ya uzio wa shule, lakini baada ya MWAUWASA kutujengea vyoo vya kisasa, hali imebadilika kwani tunajisafisha vizuri kila tunapomaliza kwenda haja kwakuwa vyoo hivi vina mfumo mzuri wa majisafi.





MJINI KATI MAMBO NI MOTO

Hayawi hayawi sasa yamekua! Hatimaye Kanda ya Mjini Kati imeongoza kwa mara nyingine tena kwenye mashindano ya utendaji kazi kwa vigezo vya mauzo na makusanyo ya maduhuli kwa mwezi Novemba, 2018.

Hii ni mara pili kwa Kanda hiyo kuibuka na ushindi kwa miezi miwili mfululizo yani Oktoba na Novemba, 2018.

Katika mpambano huo mkali wa vuta nikuvute Kanda ya Mjini Kati imeibuka na ushindi wa asilimia 95.16 ikifuatiwa na Nyegezi asilimia 92.46; Nyakato asilimia 91.29 na Kanda ya Makongoro kushika mkia kwa kupata asilimia 89.79.

Hata hivyo ushindi huo umeshuka kwa kiwango fulani ilikinganishwa na mchuano wa Mwezi Oktoba ambapo

Kanda ya Mjini Kati iliibuka na ushindi kwa kupata asilimia 97.76 ikifuatiwa na Kanda ya Nyakato asilimia 96.90, Kanda ya Makongoro asilimia 94.96 na mwisho ni Kanda ya Nyegezi asilimia 92.37.

Ikumbukwe kwamba mfumo huo wa upimaji wa utendaji kwa watumishi ulizinduliwa rasmi Agosti mwaka huu na Katibu Mkuu wa Wizara ya Maji, Profesa Kitila Mkumbo ambao unapima utendaji wa watumishi kikanda kupitia kanda zake mbazo ni Makongoro, Nyegezi, Nyakato na Kanda ya Mjini Kati.

Mashindano hayo yamelenga kuongeza makusanyo, kuongeza mauzo ya maji lakini pia kuhakikisha maji yanafika kila kona ya jiji la Mwanza na viunga vyake kwa maana ya usambazaji wa maji, kupunguza upotevu wa maji sambamba na kuhakikisha wateja wote wanaunganishwa kwenye mfumo wa maji.

Matokeo rasmi ya ushindani wa Kanda ni kama ifuatavyo:

1. Kati (95.16%)

2. Nyegezi (92.46%)

3. Nyakato (91.29%)

4. Makongoro (89.79%)

Hivyo **Kanda ya Kati** wameongoza kwa matokeo ya mwezi **Novemba 2018**.

NOTE: MWAUWASA News Bulletin inawapongeza kwa dhati. Hongereni sana muhimu ni kuhakikisha Mwezi Desemba nao unamalizika kwa ushindi.





DC NYAMAGANA AIPONGEZA MWAUWASA

Kamati ya Ulinzi na Usalama Wilaya ya Nyamagana imeipongeza Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Jijini Mwanza (MWAUWASA) kwa usimamizi mahiri wa miradi inayotekeleza.

Pongezi hizo zimetolewa na Mwenyekiti wa Kamati ya Ulinzi na Usalama na Mkuu wa Wilaya Nyamagana, Dkt Philis Nyimbi Desemba 6, 2018 wakati wa ziara ya Kamati kwenye miradi ya maji inayotekelezwa wilayani humo na MWAUWASA.

Mara baada ya kukamilisha ziara, Dkt. Nyimbi alisema amefurahishwa na utekelezwaji wa miradi ya maji kwenye wilaya ya Nyamagana na aliipongeza MWAUWASA kwa ubunifu wa hali ya juu wa miradi mbalimbali ya maji inayoendelea kujengwa.

"Nimetembea nimejionea namna mnavyopambana katika kusimamia hii miradi ya maji. MWAUWASA inatekeleza ilani ya Chama cha Mapinduzi kwa vitendo. Ninawapongeza sana kazi yenu ni nzuri na inaridhisha," alisema.

Mbali na pongezi hizo, Dkt. Nyimbi aliwataka wananchi kuhakikisha miradi hiyo inatunzwa kwa manufaa yao na vizazi vijavyo na alisisitiza kwamba ni jukumu la kila mwananchi kuwa mlinzi wa miundombinu ya maji.

"Tukumbuke maji ni uhai. Serikali imetumia fedha nyingi katika kujenga miradi hii yenye manufaa makubwa kwa wananchi wake. Ni jukumu lenu wananchi kuhakikisha miradi hii inatunzwa," alisisitiza.

Aliongeza kuwa hatua kali za kisheria zitachukuliwa dhidi ya mtu yoyote atakayebainika kuharibu miundombinu ya maji.

Naye Katibu wa Chama cha Mapinduzi Wilaya ya Nyamagana, Salum kalli alisema MWAUWASA inaongoza kwa ubora wa miradi na aliitaka kuhakikisha miradi inayoendelea kujengwa inakamilika kwa wakati.

Aidha, akizungumzia suala la gharama za umeme zinazotumika kwenye kuendesha mitambo ya kusukuma maji mara baada ya kubaini kiasi kinachotumika kulipia bili ya umeme, Kalli alisema ipo haja Wizara ya Maji na Wizara ya Nishati kukaa pamoja kutazama namna ya kupunguza gharama.

"Serikali ni moja, tunajenga nyumba moja, upo umuhimu wa kukaa pamoja kujadili kuhusiana na gharama za umeme kwa Mamlaka za Maji," alisema Kalli.



Akizungumza katika majumuisho ya ziara, Naibu Meya wa Jiji la Mwanza, Bhiku Kotecha aliipongeza Bodi ya Waku-rugenzi MWAUWASA kwa kusimamia vye-ma shughuli zinazotekelezwa na Mamlaka.

Kotecha alisema mbali na gharama ya umeme kuwa juu lakini MWAUWASA haijawahi kushindwa kulipa bili zake, jambo ambalo anasema linatokana na usimamizi mahiri wa Bodi sambamba na watendaji wa Mamlaka hiyo chini ya uongozi wa Mkurugenzi wake Mhandisi Anthony Sanga.

"Mhandisi Sanga anajitahidi sana kuisimamia MWAUWASA; jitihada zake sote tunazona; anastahili pongezi yeye na anaowaongoza," alisema Kotecha.

Kwa upande wake Mkurugenzi Mtendaji wa MWAUWASA, Mhandisi Anthony Sanga alieleza kuhusiana na miradi inayojengwa chini

ya mpango wa Uboreshaji wa Huduma ya Maji katika Jiji la Mwanza hususan kwa wakazi wa maeneo ya miinuko.

Alifafanua kwamba mpango huo unatekelezwa kwenye wilaya ya Nyamagana na Itemela na kwamba unahusisha ujenzi wa matenki; Upanuzi wa Usambazaji maji kupitia ulazaji wa mabomba mapya; Ukarabati wa Mtandao wa Usambazaji maji kupitia ubadilishaji wa bomba za zamani na kuweka mpya na Upanuzi na Uboreshaji wa Nfumo wa Majitaka.

Aidha, Mhandisi Sanga aliipongeza Kamati ya Ulinzi na Usalama Wilaya ya Nyamagana kwa kufanya maamuzi ya kutembelea miradi ya maji inayotekelezwa kwenye wilaya hiyo.

Maeneo yaliyotembelewa na ujumbe huo ni Chanzo cha Maji cha Capri-point, Ujenzi wa Matenki ya Nyegezi na Bugarika na mradi wa Majitaka (Simplified Sewerage) Mabatini.



MATUKIO MBALIMBALI KATIKA PICHA





Habari katika picha...



Kutoka kushoto, Waziri wa Maji, Mhe. Profesa Makame Mbarawa (Mb), Naibu Katibu Mkuu, Mhandisi Emmanuel Kalobelo pamoja na Kaimu Mkurugenzi wa Maji Mijini, Mhandisi Mary Mumghamba katika moja ya vikao na Waandishi wa Habari (hawapo pichani)



Katibu Mkuu Wizara ya Maji, Profesa Kitila Mkumbo (kulia) akishiriki kuchimba mtaro katika eneo la Kijiji cha Bushing'we Halmashauri ya Msalala ambapo bomba la maji la mradi wa maji wa Shinyanga na Geita (JWPP) litapita.



Waziri wa Maji, Mhe. Profesa Makame Mbarawa (Mb) akiwa na Naibu Waziri wa Maji, Mhe. Jumaa Aweso (Mb) kwenye moja ya mkutano na waandishi wa habari (hawapo pichani)



ZIARA YA BODI YA WAKURUGENZI MWAUWASA

Bodi ya Wakurugenzi ya Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Jijini Mwanza (MWAUWASA) imefanya ziara ya siku tano kwenye mamlaka tatu za maji ambazo ni Dodoma (DUWASA), Iringa (IRUWASA) na Mbeya UWSA lengo likiwa ni kujifunza na kubadilishana uzoefu.

Ziara hiyo ilianzia DUWASA na ilihitimishwa kwa kutembelea Mbeya UWSA ambapo wajumbe walipata fursa ya kutembelea maeneo mbalimbali ya mnyororo mzima wa utoaji huduma ya maji ambayo ni kuanzia kwenye vyanzo vya maji hadi kwa mtumiaji wa mwisho.

Aidha, masuala mbalimbali yalijadiliwa kwa lengo la kubadilishana uzoefu na kutafuta ufumbuzi wa pamoja wa changamoto zinazozikabili mamlaka za maji nchini ili kufikia azma ya kupanua wigo wa usambazaji wa majisafi na salama kwa wananchi.

Kwa nyakati tofauti, katika majadiliano baina ya wajumbe wa MWAUWASA na wenyeji wao, ilipendekezwa mamlaka ziandae utaratibu wa kubadilishana uzoefu katika utekekezaji wa shughuli zao ili kuleta ufanisi zaidi hasa ikizingatiwa kwamba baadhi ya changamoto kwenye utekelezaji wa miradi ya maji kote nchini zinafanana.

Majadiliano hayo vilevile yaligusia suala zima la wizi wa mita za maji ambao umezikumba mamlaka nyingi nchini na huku baadhi ya mamlaka zikionyesha kufanikiwa kuliko zingine na hivyo ilipendekezwa watumishi wajikite katika suala hili ili kuona ni namna gani wengine wamefanikiwa.

Ziara hiyo ya Bodi ya MWAUWASA kwenye mamlaka hizo, vilevile ilihusisha baadhi ya watumishi wa MWAUWASA kutoka vitengo mbalimbali ambao waliambatana na wajumbe wa Bodi.



Wajumbe wa Bodi na baadhi ya watumishi wa MWAUWASA walipotembelea chanzo cha maji cha Mzakwe Jijini Dodoma wakimsikiliza mtaalam (hayupo pichani) akiwapatia maelezo ya shughuli zinazofanyika maeneo hayo.



Wajumbe wa Bodi ya wakurugenzi MWAUWASA walipotembelea tenki la kuhifadhi maji lililopo maeneo ya Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM) wakimsikiliza Mkurugenzi Mtendaji wa DUWASA, Mhandisi David Pallangyo (kulia). Kutoka kushoto ni, Edith Mudogo, Frank Masasi, Denisa Pagulla na Ellen Bogohe



Wajumbe wa Bodi za Wakurugenzi MWAUWASA na wenyeji wao Mbeya UWSA walipotembelea chanzo cha maji cha Iyumwe.



Wajumbe wa Bodi na baadhi ya watumishi wa MWAUWASA walipotembelea chanzo cha maji Chemchemi ya Kitwiro Mkoani Iringa.



MAMLAKA ZA MAJI NCHINI WAASWA KUSHIRIKIANA



Wajumbe wa Bodi za Wakurugenzi MWAUWASA na IRUWASA wakiwa katika picha ya pamoja na baadhi ya watumishi wa mamlaka hizo mara baada ya kukamilisha ziara ya kwenye maeneo mbalimbali ya mnyororo mzima wa huduma ya maji Mkoani Iringa.

Watumishi Mamlaka za Maji nchini wameaswa kushirikiana ili kuboresha shughuli zao sambamba na kuongeza kasi ya usambazaji wa huduma ya maji kwenye maeneo yao.

Makamu Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Jijini Mwanza (MWAUWASA), Edith Mudogo ametoa wito huo hivi karibuni Jijini Dodoma wakati wa Ziara ya Wajumbe wa Bodi hiyo kwenye Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mjini Dodoma (DUWASA).

Mudogo alisema ni vyema watumishi wa Mamlaka mbalimbali nchini wakawa na utaratibu wa kubadilishana uzoefu katika utekelezaji wa shughuli zao ili kuleta ufanisi zaidi hasa ikizingatiwa kwamba baadhi ya changamoto kwenye utekelezaji wa miradi ya maji

kote nchini zinafanana.

"Watendaji inabidi mtazame namna ya kubadilishana uzoefu wa utekelezaji wa miradi ya maji. Baadhi ya changamoto mnazokutana nazo unakuta wengine nao walikuwa nazo lakini walifanikiwa kuzitatua na hii itawasaidia nanyi kuwa na utatuzi wa haraka kwa kujifunza kutoka kwa wengine," alisisitiza.

Mudogo alitolea mfano suala la wizi wa mita za maji ambapo alisema baadhi ya mamlaka tayari zimeonyesha kufanikiwa katika kudhibiti hali hiyo na alisema ni vyema mamlaka zikawa na utaratibu wa kubadilishana uzoefu wa utatuzi wa changamoto kupitia njia mbalimbali ikiwemo ya kutembeleana.

Kwa upande wake Mwenyekiti wa Bodi ya DUWASA, Balozi Job Lusinde alipendelea kwa siku za baadaye kukaandaliwa utaratibu wa kubadilishana watumishi miongoni mwa

mamlaka za maji kwa muda ili kubadilishana uzoefu.

Balozi Lusinde alisema kila mamlaka inayo maeneo ambayo imefanikiwa kuliko nyingine na hivyo ni jambo la busara mamlaka zingine zikatamia uzoefu huo wa mafanikio kutoka kwa wataalam wa mamlaka husika ili nao kupiga hatua.

"Unaweza ukakuta kuna mamlaka imepiga hatua kwenye suala la majitaka na hivyo sio jambo baya kuazima watendaji wa mamlaka hiyo ili kufika huko walipo wengine," alisema Balozi Lusinde.

Aidha, ziara hiyo ya Bodi ya MWAUWASA ilihusisha baadhi ya watumishi wa MWAUWASA kwa lengo la kujifunza utekelezaji wa majukumu sambamba na kubadilishana uzoefu kiutendaji.



Wajumbe wa Bodi za Wakurugenzi MWAUWASA na wenyeweji wao Mbeya UWSA walipotembelea eneo la kutibu maji la Swaya Jijini Mbeya. Wa pili kushoto ni Mkurugenzi Mtendaji MWAUWASA, Mhandisi Anthony Sanga.



Wajumbe wa Bodi za Wakurugenzi MWAUWASA na wenyeweji wao Mbeya UWSA walipotembelea chanzo cha maji cha Nzowwe. Wa tatu kutoka kushoto ni Mwenyekiti wa Bodi MWAUWASA, Christopher Gachuma.



TUZO



Meneja Fedha wa MWAUWASA, Petro Nyanjige akikabidhi rasmi kwa Mkurugenzi Mtendaji wa MWAUWASA Tuzo ya Ushindi katika utunzaji bora wa mahesabu ya fedha kwa Mwaka 2017 ambayo alipokea kwa niaba yake ambapo MWAUWASA iliibuka mshindi wa pili. Tuzo hiyo imetolewa Desemba, 2018 na Bodi ya Taifa ya Wahasibu na Wakaguzi (NBAA).



OFA OFA OFA



JE ULISITISHIWA HUDUMA YA MAJI KWA KUSHINDWA KULIPA BILI...???

Sikia hii...

MAMLAKA YA MAJISAFI NA USAFI WA MAZINGIRA JIJINI MWANZA (MWAUWASA) INAKULETEA OFA KABAMBE YA 'RUDISHA BURE LIPA KWA AWAMU'

TUNAPENDA KUWATANGAZIA WATEJA WOTE WALIOSITISHIWA HUDUMA YA MAJI KUTOKANA NA MALIMBIKIZO YA MADENI KUWA KATIKA KUSHEREHEKEA MSIMU WA SIKUKUU ZA KRISMASI NA MWAKA MPYA SASA WATAJESHEWA HUDUMA YA MAJI BURE BILA FAINI YOYOTE ENDAPO WATAJITOKEZA KULIPA MADENI YAO KWA AWAMU.

OFA HII HAITAHUSIKA NA WATEJA WATAKAOKATIWA MAJI MWEZI DESEMBA 2018 NA JANUARI 2019.

KWA MAELEZO NA UTARATIBU TAFADHALI FIKA KWENYE OFISI YA MWAUWASA ILIYO KARIBU NAWA.

OFA HII NI MAALUM MSIMU HUU WA SIKUKUU ZA KRISMASI NA MWAKA MPYA NA MWISHO NI TAREHE 31 JANUARI, 2019.

NDUGU MTEJA 'RUDISHA BURE LIPA KWA AWAMU'

TUNAWATAKIA WATEJA WETU MSIMU MZURI WA SIKUKUU ZA KRISMASI NA MWAKA MPYA

**Imetolewa na:
Ofisi ya Uhusiano MWAUWASA.**



Na Lawrence Temba

Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini

Wakati Serikali inaweza katika miradi ya maji nchini, ni jukumu la kila mwananchi kuwa mlinzi wa miundombinu ya maji pamoja na vyanzo vya maji. Hatua hii itasaidia miradi ya maji inayojengwa kuwa endelevu.

Maji ni rasilimali muhimu kwa ustawi wa jamii na maendeleo ya kiuchumi, na rasilimali hii haina mbadala. Tafti zinaonyesha kuwa Tanzania inakadiriwa kuwa na rasilimali za maji juu ya ardhi zenye kilomita za ujazo 92.27 na chini ya ardhi kilomita za ujazo 38. Kupitia rasilimali hii muhimu nia na lengo kuu la Serikali ni kuhakikisha wananchi wanapata huduma ya majisafi na salama jirani na makazi yao.

Ni wazi kuwa rasilimali za maji zinahitaji kulindwa na kutunzwa kwa sababu hazina mbadala. Ni jambo la msingi kila mwananchi akielewa umuhimu wa utunzaji wa mazingira kwasababu kila mmoja anahitaji kutumia maji kwa shughuli mbalimbali za maendeleo.

Naibu Waziri wa Maji Mhe. Jumaa Aweso (Mb) hivi karibuni akiwa katika ziara ya kikazi ya mradi kwa mradi mkoani Manyara aliwataka viongozi mbalimbali katika jamii kutoa elimu na kuwashirikisha wananchi katika miradi ya maji, hususan kulinda vyanzo vya maji na miundombinu yake.

Waziri Aweso akiongea na wakazi wa eneo la Waranga, Katesh alisema ni jambo la msingi kulinda vyanzo vya maji ili kuwa na uhakika wa huduma endelevu ya majisafi na salama na kusisitiza kuwa ili kutekeleza mradi wa maji ni lazima kuwepo na chanzo cha uhakika cha maji kuweza kutoa huduma ya majisafi na salama kwa wananchi muda wote.

Mhe. Aweso alisema kulinda vyanzo vya maji ni jukumu la kila mwananchi kwa sababu maji hayana mbadala, na kila mtu anayahitaji kila siku, kila wakati, iwe nyumbani, ofisini, shuleni au katika shughuli nyingine ikiwemo kilimo, ufugaji na ujenzi.

Hata hivyo, Waziri Aweso akiweka jive la msingi la mradi wa maji wa mji wa Katesh uliojengwa na Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira mjini Babati (BAWASA) aliwataka wakandarasi kufanya utafiti ili kupata vyanzo vya maji vya uhakika kabla ya kuweka miundombinu. Alisema hatamvumilia mkandarasi atakayewadanganya wananchi kwa kufanya kazi kwa ulaghai wakati hajatafiti kupata chanzo cha uhakika na chakutosha cha maji.

Waziri Aweso alisema hadi mwezi Septemba 2018 takwimu zinaonyesha katika mkoa wa Manyara upatikanaji wa maji vijijini ulikuwa asilimia 52 na Babati mjini asilimia 75, ilhali mkoa huo una vyanzo vya maji mbalimbali ikiwamo visima virefu 296, visima vifupi 320, chemchemi 93 na mabwawa 123.

Mkoani manyara, Waziri Aweso alibaini baadhi ya vyanzo vya maji kuvamiwa kwa shughuli mbalimbali, ikiwamo kilimo, ufugaji na kazi za kufyatua tofali hali inayohatarisha upatikanaji wa maji katika vyanzo hivyo kutokuwa endelevu, na hivyo kazi hizo za kibinadamu kuchochea kukuza adha ya upatikanaji majisafi na salama.

MAKALA MAALUM

TULINDE VYANZO VYA MAJI-AWESO



Waziri wa Maji Mhe. Profesa Makame Mbarawa (Mb) akikagua mradi wa maji wa Nansio. Vyanzo vya maji vya uhakika ni muhimu katika kuhakikisha wananchi wengi wanapata huduma ya maji safi na salama kwa uhakika. Mradi wa maji wa Nansio unatoa maji katika Ziwa Victoria, na umetekelezwa kupitia Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Jijini Mwanza (MWAUWASA).

Waziri Aweso aliwaelekeza viongozi wote kuanzia ngazi za mtaa mkoani Manyara kulinda na kuelimisha kuhusu umuhimu wa kutunza vyanzo vya maji kwa maendeleo ya kila mwananchi. Aidha, alikumbusha hairuhusiwi kufanya shughuli yoyote ndani ya mita 60 kutoka chanzo cha maji.

Pamoja na hilo, Waziri Aweso alitumia wasaa huo akiwa katika mradi wa maji wa Gehandu mkoani Manyara kuwaelekeza wataalam wa maji kote nchini, kutokubali wakandarasi kuweka miundombinu ya maji kabla ya kupata chanzo cha uhakika cha maji. Alisema serikali inapotoa fedha kutekeleza mradi wa maji, maana yake ni wananchi kusubiri maji hayo na sio jambo jingine.

Kuhusu kulinda vyanzo vya maji, Afisa Rasilimalimaji kutoka Bonde la kati Bw. Lazaro Msengi, alisema ni muhimu kuweka mipaka katika vyanzo vya maji ili kuepuka shughuli za aina yoyote katika maeneo hayo.

Bw. Msengi alisema pamoja na mabadi-liko ya tabia nchi, rasilimalimaji inaisha kwa kasi ya kutisha. Hivyo, endapo shughuli za kilimo katika vyanzo vya maji, ikiwamo kuingiza mifugo katika vyanzo vya maji hazitasitishwa mara moja, hali hiyo inahatarisha uendelevu wa vyanzo vya maji na rasilimalimaji.

Hata hivyo, Diwani wa Minjingu Mhe. Michael Milao alisema jambo la msingi ni kwa wataalam katika sekta ya maji kuwashirikisha wananchi katika masuala utunzaji wa mazingira, hasa vyanzo vya maji katika maeneo mbalimbali nchini. Alisema kuwa wananchi wakishirikishwa na kupewa elimu ya kutosha kila jambo litakaa sawa na kuongeza kutokuwa na elimu na taarifa za kutosha kunasababisha baadhi ya wananchi kutofuata taratibu zinazotakiwa.

Suala hili la elimu linaungwa mkono na Mwenyekiti wa Kijiji cha Tsamam Bw. Jumanne Selemani aliyesema

kutoshirikishwa kwa wananchi na kupewa elimu ni tatizo kusisitiza mbinu za utunzaji wa mazingira, na kulinda vyanzo vya maji ni la muhimu ikiwamo ufugaji wa kisasa.

Wataalam katika sekta ya maji wanasema kuwa shughuli za kibinadamu zinasababisha kwa kiwango kikubwa vyanzo vya maji kukauka au kutoa maji kwa msimu. Hivyo, kutoa elimu ya utunzaji vyanzo vya maji ili kuepuka kuvamiwa kwa shughuli mbalimbali za kibinadamu ni muhimu.

Pamoja na hilo, ili kuhakikisha miradi ya maji inakidhi mahitaji kwa kufikia malengo ya serikali Mkurugenzi Mtendaji wa BAWASA Mhandisi Yazidi Msuya anasema ni vizuri wataalam katika sekta mbalimbali wakishirikiana ili kubaini changamoto na kuzifanyia kazi mapema ili kuhakikisha wananchi wanapata huduma ya majisafi na salama wakati wote na kwa uhakika.



Naibu Waziri wa Maji Mhe. Jumaa Aweso (Mb) akiwa katika ziara ya mradi kwa mradi, akishiriki kazi ya kuchimba mtaro ili kupata nafasi ya kurekebisha bomba la kusambaza huduma ya majisafi kwa wakazi wa Haydom, eneo la stendi ya zamani, mkoani Manyara hivi karibuni.



TUTAKUFIKIA, TUTAKUSIKILIZA, TUTAPATA UFUMBUZI WA PAMOJA



EWE MWANANCHI
tunakufuata hapo ulipo
kupitia programu yetu ya:

**"Zungumza
na
MWAUWASA"**



mwauwasa



0800110023



mwauwasatz

Zungumza na **MWAUWASA** ni programu maalum iliyoanzishwa na Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Jijini Mwanza (MWAUWASA) ili kujadiliana na wananchi juu ya kero walizonazo kwenye suala zima la huduma ya maji.

Programu hii ni endelevu na inaendeshwa kwa mpango wa mikutano ambayo itaitishwa na Wenyevitwa wa Mitaa kwa kushirikiana na **MWAUWASA**.

Faida ya Programu hii ni pamoja na:
Mwananchi kupata fursa ya kueleza kero uliyonayo kuhusiana na suala zima la huduma ya maji;
Kutakuwa na utatuzi/ufumbuzi wa pamoja wa kero;
Mwananchi kupata elimu ya masuala mbalimbali yanayohusu maji; na
Mwananchi kupata fursa ya kuelewa shughuli zinazofanywa na **MWAUWASA**.

Ewe Mwananchi ni wakati wako sasa kutueleza kero zako, tunakuja kuzungumza nawe.



TAHADHARI

MAMLAKA YA MAJISAFI NA USAFI WA MAZINGIRA JIJINI MWANZA (MWAUWASA) INAWAKUMBUSHA WATEJA WAKE NA WANANCHI KWA UJUMLA MALIPO YOTE IWE KULIPIA BILI, KULIPIA GHARAMA YA KUUNGANISHIWA HUDUMA AMA KULIPA FAINI YAFANYIKE KWA NJIA YA MITANDAO YA SIMU, BENKI AMA WAKALA WA BENKI

NDUGU MTEJA KUFANYA MALIPO KWA NJIA ZINGINE IKIWEMO KUMPATIA MTU FEDHA TASLIMU AKA-KULIPIE (HATA KAMA MTU HUYO NI MTUMISHI WA MWAUWASA) NI KINYUME CHA TARATIBU.

MAMLAKA HAITAHUSIKA NA SUALA LOLOTE NJE YA UTARATIBU WA MALIPO ULIOELEZWA HAPO JUU.

KWA TAARIFA ZAIDI PIGA NAMBA: 0800110023 (BURE)



BODI YA WAKURUGENZI,
MENEJIMENTI NA WATUMISHI WA
MAMLAKA YA MAJISAFI NA USAFI WA
MAZINGIRA JIJINI MWANZA
(MWAUWASA) INAPENDA
KUWATAKIA WATEJA WAKE NA
WATANZANIA KWA UJUMLA HERI YA

**KRISMASI NA
MWAKA MPYA 2019**



2019